

**HOTUBA YA MKURUGENZI MKUU (NEMC), Eng. B.T. Baya -
KATIKA HAFLA YA MSAFARA WA WAENDESHA BAISKELI
WA DAR ES SALAAM KAMA NJIA YA KUPAMBANA NA
MABADILIKO YA TABIANCHI, JUMAPILI TARHE
10/10/2010 KATIKA VIWANJA VYA
MNAZI MMOJA – DAR ES SALAAM**

Ndugu Mwenyekiti wa UWABA
Umma wa Wapanda Baiskeli (UWABA),
Mtandao wa Forum CC (Tanzania Civil Society Forum on CC),
Mwakilishi wa Hip Hop Music Group
Ndugu Wananchi wote,
Ndugu Wanahabari (Business Times),
Mabibi na Mabwana.

Awali ya yote napenda kuushukuru uongozi wa UWABA na Forum CC kunipa nafasi (Mgeni Rasmi) ili kuweza kutoa salamu na ujumbe mfupi katika tukio hili muhimu sana hapa kwetu leo. Napenda vilevile kuungana na wasemaji waliotangulia kuwashukuru wote kwa kujitokeza kushiriki hafla hii muhimu na hususan wote walioshiriki kuendesha baiskeli ikiwa ni ishara ya kubambana na mabadiliko ya Tabianchi. Kitendo cha kuendesha baiskeli inaashiria mwamko miongoni mwetu na njia mojawapo nzuri ya kuhamasisha wananchi kuhusu umuhimu wa matumizi ya baiskeli kwa faida ya afya zetu na hifadhi ya mazingira

hususan madhara yanayosababishwa na mabadiliko ya tabianchi (climate change).

Ndugu wananchi, nachukua fursa kutoa pongezi nyingi kwa UWABA na Forum CC kwa kubuni njia hii sahihi ya kuelimisha umma kwa vitendo, ambayo inahamasisha wananchi kujenga afya nzuri kwa njia ya mazoezi ya baiskeli, na kama njia ya kupambana na mabadiliko ya tabianchi. Wananchi wenzangu, sikukuu hii ya vitendo (kama vile kuendesha baiskeli tulioshirikiana leo nk), ni tukio la kidunia linalofanywa na wakereketwa wa mazingira. Lengo kuu ni kuhamasisha dunia kuelewa na kushiriki vitendo vya kupambana na mabadiliko ya tabianchi kwa kupunguza uzalishaji wa gesi joto duniani. Kwa mujibu wa taarifa za tovuti (*internet*), nchi zipatazo 188 zimepanga kushiriki kwa njia mbaliimbali ikiwemo kutoa salamu na kufanya kwa vitendo (practical actions) - matukio zaidi ya 7,000 kuhusu hifadhi ya mazingira.

Ndugu Wananchi,

Aidha, nitumie fursa hii kuwashukuru Wandaaji wa shughuli hizi leo kwa kunialika kwa niaba ya sekta ya mazingira kuwa mgeni rasmi. Naamini hii imetokana na kuongezeka kwa uelewa juu ya masuala ya mazingira na umuhimu wa hifadhi ya mazingira kwa jumla. Sheria yetu ya Mazingira (2004) imetoa wajibu wa hifadhi ya mazingira kwa kila mwananchi.

Tatizo la mabadiliko ya tabianchi ni moja ya vipaumbele vya Serikali, hivyo Ofisi ya Makamu wa Rais na Baraza la Mazingira (NEMC) ni wadau wenu wakubwa. Napenda kusema shughuli hii hizi ni zetu na hatuna budi kushiriki na kuzipa msukumo (support) ipasavyo.

Ndugu Wananchi,

Naomba nitoe maelezo mafupi kuhusu faida ya matumizi ya baiskeli. Historia inaonyesha baiskeli zilianza kutumika kabla ya magari. Makampuni makubwa duniani (yakiwemo *Peugeot, Opel, Humber & Rover*) zilitengeneza baiskeli kabla ya magari. Wakati wa vita ya dunia ya kwanza inakisiwa kulikuwa na baiskeli zaidi ya Milioni 9.0 katika bara la Ulaya na Marekani. Faida kuu za kutumia baiskeli kama njia ya usafiri kulinganishwa na magari ni zifuatazo:

- Ni rahisi kuinunua na kuihudumia na pia inaweza kutumika katika mazingira yasiyokuwa na barabara rasmi. (It is social means of transport).
- Ni rahisi kuiendesha na inaokoa gharama na muda wa usafiri hususan katika masafa mafupi ndani ya miji na vitongoji.
- Inachukua nafasi kidogo katika barabara na maegesho, hivyo kuruhusu watumiaji wengi zaidi wa nafasi zilizopo.

- Haina kelele, haitumii mafuta, haichafui mazingira, na haihatarishi usalama wa watumiaji wengine wa njia au barabara.

Hata hivyo tukumbuke kuwa hakuna kitu kisichokuwa na kasoro, matumizi ya baiskeli yasipozingatiwa vizuri inaweza kusababisha vifo na uharibifu. Nchi za Uingereza na Uturuki (Turkey) ziliwahi kutoa takwimu za vifo vilivyosababishwa na baiskeli. Ongezeko kubwa lilionekana huko Uingereza (1954-1988) na vifo 729 vilitokea huko Uturuki na 9 Norway (1984). Miundombinu lazima izingatie usalama wa waendesha baiskeli, ili kupunguza au kuepuka madhara haya. Je takwimu ya Tanzania ikoje?

Ndugu Wananchi,

Nimesema baiskeli ni njia ya usafiri ambao ni rafiki wa mazingira. Tukumbuke kuwa mabadiliko ya tabianchi (climate change) ni janga la kidunia linalosababishwa na kuzagaa kwa hewa ya ukaa (*carbondioxide*) kwenye hewa katika anga ya dunia, kutokana na kuchoma mafuta, makaa ya mawe na gesi (fossil fuel) katika magari, viwanda, ndege na uzalishaji wa umeme.

Juhudi za kupunguza au kuleta suluhisho la mabadiliko ya tabianchi ni za kudunia, kitaifa na kwa kila mmoja wetu kwa nafasi yake. Juhudi hizi zinahusu pia jinsi tunavyosafiri na

kusafirisha. Matumizi ya baiskeli au uendeshaji wa baiskeli unahamasishwa kama hatua inayochangia mapambano dhidi ya tatizo la mabadiliko ya tabianchi (kwa punguza uzalishaji wa gesi joto – GHG). Nimefurahishwa kwa ujumbe ulio katika mabango na T-shirts zetu za kupunguza uzalishaji wa gesi hizo.

Ndugu Wananchi,

Mabadiliko ya tabianchi ni tatizo kubwa kitaifa na kimataifa hivyo wote linatuhusu katika kulitafutia mbinu za kupunguza madhara yatokanayo na mabadiliko ya tabianchi. Baadhi ya shughuli za binadamu zinazochochea kasi ya kuongezeka kwa tatizo la mabadiliko ya tabianchi ni pamoja na; uzalishaji viwandani, usafiri, uchomaji moto misitu, ukataji miti ovyo na matumizi ya mafuta katika shughuli mbalimbali za uchumi.

Madhara yanayosababishwa na mabadiliko ya tabianchi ni pamoja na: kuongezeka kwa joto duniani, kuongezeka kwa magonjwa kama malaria, kuongezeka kwa kina cha bahari, kupungua kwa mvua, matukio ya mafuriko na ukame. Hapa kwetu Tanzania tumeanza kushuhudia mabadiliko ya tabianchi katika maeneo kadhaa:

- **Ukame** wa mwaka 2009 katika mikoa ya Arusha, Kilimanjaro - mifugo mingi ilikufa na mazao kukauka na kusababisha njaa – kuchochea umaskini miongoni mwa jamii nchini.

- **Kuongezeka kwa joto** kumeshababisha theluji katika mlima Kilimanjaro kupungua kwa zaidi ya silimia 50%, kuzama kwa visiwa vya wavuvi vya Maziwe (Pangani) na Fungu la Nyani (Zanzibar).
- **Kuongezeka kwa malaria** katika maeneo ambayo hayakuwa na malaria kama Arusha, Mbeya, Lushoto na Njombe sasa yana malaria.
- Aidha, Ziwa Rukwa limepungua kwa zaidi ya asilimia 80.

Serikali na wananchi kwa pamoja hatunabudi kushirikiana ili kuweka mikakati ya kupunguza na kukabiliana na mabadiliko haya.

Ndugu Wananchi,

Matumizi ya baiskeli yamepongezwa duniani kote kuwa njia bora ya usafiri unaopunguza kasi ya mabadiliko ya tabianchi. Nchi za wenzetu ya Ulaya na Marekani inayo miji inayojulikana kwa usafiri baiskeli na kama njia ya kuhifadhi mazingira. Mwamuko wa Wananchi wetu, hasa walioshiriki tukio hili la kuendesha baiskeli leo ni la muhimu na linastahili kupongezwa na kuhamasishwa kwa nguvu zote.

Juhudi hizi zinatia moyo na kufurahisha sana kwani takwimu zinaonyesha vijana wengi hasa mijini ndio watumiaji wakubwa wa magari hata kwa mwendo mfupu ambao wangetembea kwa miguu au kuendesha baiskeli. Hivyo elimu hii ikisambaa kwa

vijana na watumiaji wengine wa magari na pikipiki tutaweza kupunguza matumizi ya vyombo hivyo na hivyo kupunguza madhara yake ambayo idadi yake inazidi kuongezeka siku hadi siku (zaidi 5.0.milioni yanatumika barabarani).

Aidha, tukumbuke kuwa, katika miaka ya karibuni kumekuwa na ongezeko kubwa la magari na pikipiki hasa sehemu za mijini, na pia katika kipindi kifupi kumekuwa na ongezeko kubwa hivyo kuongeza matumizi ya mafuta (petroli) ambayo yanachangia kwa kiasi kikubwa uchafuzi wa hewa na hivyo kuongeza madhara yanayochochea mabadiliko ya tabianchi.

Tatizo hili linakuwa kubwa zaidi ukizingatia kuwa magari au vyombo vingi vya usafiri vinavyoagizwa kutoka nje ya nchi ni vichakavu. Uchakavu huu unasababisha matumizi makubwa ya mafuta , gesi na makaa ya mawe na kuzalisha moshi wenye kiwango kikubwa cha hewa ya ukaa na hewa nyingine ambazo husababisha mabadiliko ya tabianchi na kuathiri afya ya jamii.

Ndugu Wananchi,

Kama tabia tutajenga utamaduni wa kuendesha baiskeli badala ya magari na pikipiki kama usafiri mbadala hasa sehemu za mijini, tutakuwa tumepiga hatua kubwa katika kupambana na mabadiliko ya tabianchi. Kwa kufanya hivyo

tutakuwa tumepunguza matumizi ya mafuta ambayo huligharimu Taifa letu fedha nyingi, tutapunguza uchafuzi wa hewa, tutapunguza msongamano wa magari na pikipiki jambo ambalo limekuwa kero kubwa katika miji yetu inayoendelea kupanuka na kusongamana kila siku.

Aidha, ni dhahiri kuwa kuendesha baiskeli kunaimarisha afya, tukizingatia kuwa watu wengi hasa wa mijini tumekuwa na tabia ya kutofanya mazoezi na muda wote na kutumia magari hata kwa umbali mfupi jambo ambalo ni hatari kwa afya zetu. Kwa kutumia baiskeli tutakuwa tumepata mazoezi ya kutosha kuboresha afya zetu.

Ndugu Wananchi,

Serikali inatambua changamoto zinazokabili waendesha baiskeli kama njia ya usafiri hasusan katika miji yetu nchini. Baadhi ya changamoto hizo ni pamoja na kuwa: ubora, matumizi na usalama wa barabara hazikidhi mahitaji (k.m. mashimo, mitaro na misingi isiyopitika) na uvukaji mgumu katika taa na uvunjaji sheria za barabara, hivyo kuhatarisha usalama wa waendesha baiskeli. Ni matumaini yangu kuwa vyombo vya serikali na wadau wa masuala ya usafiri hasa mijini watahughulikia changamoto hizi ili kuboresha mazingira ya usafiri wa baiskeli nchini.

Ofisi ya Makamu na Baraza la Mazingira (NEMC) tutatoa ushirikiano wa hali ya juu kwa sekta na wadau wa usafiri ili kuhamasisha matumizi ya baiskeli nchini kama njia ya usafiri ambao ni rafiki wa mazingira. Kwa mfano miji mingi ya Ulaya na Marekani inajulikana kama "Bicycle Cities" (km. Davis City huko California State). Naamini kabisa kuwa wote tumeguswa na suala hili na tutaliendeleza.

Aidha, ni mategemeo ya serikali kuwa juhudi zilizoonyeshwa mwaka huu katika kuhamasisha matumizi ya baiskeli na uelewa juu ya masuala ya mazingira yatadumishwa na kuongezeka zaidi siku zijazo. Nachukua fursa hii tena kuwashukuru UWABA & Forum CC kwa juhudi hizi na pongezi kwa mafanikio haya. Aidha, niwapongeze wote watakozawadiwa leo, Wanahabari na Kikundi cha musiki (Hip Hop). Kwa namna ya peke napenda kumshukuru Balozi TIM kwa kutoa hamasa kwa wapanda baiskeli na kushiriki kwake.

Ndugu Wananchi,

Mwisho, napenda kutoa wito kwa wasimamizi na waratibu wa masuala ya usafiri, na wadau mbali mbali wa mazingira na wananchi wote kwa ujumla wahamasike kupanda baiskeli badala ya magari na pikipiki tu. Tukumbuke daima **"Baiskeli ni Afya na ni rafiki wa Mazingira - Mazingira ni Uhai"**

Baada ya kusema hayo, niwashukuru kwa kushiriki kwenu na kuunga mkono juhudi za wakereketwa wenzetu duniani katika sikukuu ya vitendo kupambana na mabadiliko ya tabianchi na pia kuimarisha afya zetu.

ASANTENI SANA KWA KUNISIKILIZA